KWAYA YA MTAKATIFU KIZITO
PAROKIA YA MWENYEHERI ANUARITE MAKUBURI
+255742000089|+255713975788
kmkmakuburi
www.kmkmakuburi.co.tz
stkizitochoir@gmail.com

NINAKUPENDA EWE MWOKOZI WANGU-MWARABU

Kiitikio

Ninakupenda Ewe Mwokozi wangu, rafiki yangu mpenzi wa moyo wangu

Ukae nami daima ndani yangu, nipate nguvu rohoni siku zote.

Mashairi

1. Ninakutolea mwili na roho yangu, uzipe neema zako nipate nguvu,
   Nikae nikupendeze Mwokozi wangu, shetani muovu kamwe asinifwate.

2. Nilinde niwe imara na mwenye nguvu, nisitumbukie tena katika dhambi,
   Unionyeshe yaliyo ya heri kweli, nipate kuishi kwa kumpendeza Bwana.

3. Wewe uliye njia kweli na uzima, niongoze vema daima siku zote,
   Uniangazie mwanga palipo giza, nifike kwa Mungu Baba kwa njia yako.

4. Nakukaribisha Bwana moyoni mwangu, nijalie baraka zako Ewe Bwana,
   Hata siku ya mwisho itapowadia, niite mbinguni kwenye heri milele.